**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TANGAZO LA MWALIKO KWA VYOMBO VYA HABARI VYENYE NIA YA KUCHAPISHA AU KUTANGAZA HABARI WAKATI WA KUPIGA KURA, KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO KWENYE UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025

Kwa kuzingatia kifungu cha 26 cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa vyombo vya habari vyenye nia ya kuchapisha au kutangaza habari wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo.

Chombo cha Habari kinachohitaji kuomba kibali kinapaswa kuwa na sifa au vigezo vifuatavyo:

(i) kiwe kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016; na

(ii) kihakikishe kuwa waandishi wake wamethibitishwa na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari na wana *Press Cards* zilizotolewa na Bodi hiyo.

Maombi yawasilishwe kupitia mfumo wa usajili **Accreditation Management System (AMS)** unaopatikana kupitia kiunganishi (link) https://ams.inec.go.tz. Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe **03 Septemba, 2025 hadi 03 Oktoba, 2025.**

Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa hayatafanyiwa kazi.

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa vyombo vya habari vitakavyopewa kibali.

Limetolewa leo tarehe 03 Septemba, 2025 na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**